مَوْقِفُ الشِّيْعَةِ الإِمَامِيَّةِ الإِثْنَي عَشَرِيَّةِ

مِنَ الصُّوْفِيَّةِ

# MSIMAMO WA

## SHIA IMAAMIYYAH ITH-NAASHARIA

# DHIDI YA MASUFI


Mwandishi

Abdallah Bin Muhammad

Tarjama

Abu Halima Arafat

**Haki zote zimehifadhiwa**

**Chapa ya kwanza**

**1435h – 2014m.**

YALIYOMO


1. UTANGULIZI....................5
2. **MAKOSA YA KIITIKADI KATI YA MASUFI NA SHIA IMAAMIYYAH**....................**9**
3. **MSIMAMO WA SHIA IMAAMIYYHA KUHUSU KUPOTOSHWA KWA QUR'AN**....................**9**
4. **ITIKADI YAO KWAMBA QUR'AN SI HOJA MPAKA AJE QAYYIM (MAHDI WAO)**.....**12**
5. ITIKADI YAO KWAMBA MAIMAMU NDIO WAJUZI ZAIDI WA QUR'AN KULIKO YEYOTE.......13
6. KAULI KWAMBA SEHEMU KUBWA YA QUR'AN IMESHUKA KWAO NA KWA MAADUI ZAO.13
7. MSIMAMO WA SHIA IMAAMIYYAH DHIDI YA SUNNAH (HADITHI) ZA MTUME....................14
8. MSIMAMO WA SHIA IMAAMIYYAH DHIDI YA MASWAHABA WA MTUME....................18
9. MSIMAMO WAO DHIDI YA MAMA WA WAUMINI (WAKEZE MTUME)....................21
10. DUA YAO YA KUWALAANI MASANAMU MAWILI NA KUWALAANI AISHA NA HAFSA..........24
11. **MSIMAMO WA SHIA ITHNAASHARIA DHIDI YA MASUFI NA USUFI**....................**25**
12. MASUFI MBELE YA SHIA IMAAMIYAH NI WATU WAOVU, WAMELAANIWA, NA WAMEFUKUZWA KATIKA REHMA ZA ALLAAH....................
13. MASUFI MBELE YA SHIA IMAAMIYYAH NI MAYAHUDI WA UMMA HUU, WAPOTEVU KULIKO MAKAFIRI, NI WATU WA MOTONI NA AMALI ZAO NI AMALI ZA WATU WAOVU!!....................27
14. **MSIMAMO WA MAIMAMU WA KISHIA DHIDI YA MASUFI**....................**29**
15. IMAMU AL-SADIQ AMEWAHUKUMU MASUFI KWAMBA NI MAADUI WA AHLUL BAYT, NA MWENYE KUWAPINGA NI SAWA NA MWENYE KUPIGANA JIHAD AKIWA NA MTUME!!.........29
16. **MSIMAMO WA IMAM AL-SADIQ KWA MASUFI NA HUKUMU YAKE KWAMBA HAO NI WATU WA ITIKADI MBOVU**....................**29**
17. MSIMAMO WA IMAM MUSSA BIN JA'FAR DHIDI YA MASUFI....................30
18. MSIMAMO WA IMAM AL-RIDHWA DHIDI YA MASUFI NA HUKUMU YAKE KWAMBA HAO NI WATU WAPOTOFU NA WAJINGA, NA MWENYE KUWAPINGA NI SAWA NA ALIYEPIGANA JIHAD DHIDI YA MAKAFIRI AKIWA PAMOJA NA MTUME....................31
19. MSIMAMO WA IMAM AL-HAADI DHIDI YA MASUFI NA HUKUMU YAKE KWAMBA HAO NI MANASWARA (WAKRISTO ) NA MAJUSI (WAABUDIA MOTO) WA UMMA HUU....................32
20. MSIMAMO WA IMAM AL-'ASKARY DHIDI YA MASUFI....................33
21. MAKUBALIANO YA SHIA IMAAMIYYAH WOTE JUU YA UBATILI WA MADHEHEBU HII..........34
22. MSIMAMO WA MAULAMAA WA SHIA IMAAMIYYAH AMBAO WAMEWAPINGA MASUFI NA KUWAPA HUKUMU YA UKAFIRI NA UPOTEVU, MIONGONI HAO NI:....................35

23. SHEIKH WAO AHMAD BIN MUHAMMAD (AL-MUQADDAS AL-ARDABILIY)....35
24. SHEIKH WAO AL-MUFID....35
25. RAIS WA WANACHONI WA HADITHI NA SHEIKH WAO ABU JA'FAR AL-MAJLISIY....36
26. SHEIKH WAO NI'MATULLAAH AL-JAZAAIRIY....37
27. SHEIKH WAO SHIHAABU DDIYN AN-HAJAFIY AL-MAR'ASHIY....38
28. SHEIKH WAO MUHAMMAD BIN TWAAHIR BIN MUHAMMAD AS-SHIRAAZIY AL-QUMMI...38
29. SHEIKH WAO MUHAKIKI MUHSIN BIDARFER....39
30. SHEIKH WAO WA ZAMA HIZI MLEBANON MUHAMMAD JAMIL HAMOUD AL-'AAMILIY....39
31. **HAIFAI KUJIITA SUFI ISIPOKUWA KATIKA HALI YA KUFANYA TAQIYYAH....40**
32. **HITIMISHO....41**
33. BAADHI YA VITABU VILIVYO ANDIKWA KATIKA KUWAJIBU SHIA RAAFIDHWA....42
34. MITANDAO MUHIMU KWA AJILI YA KUWAJIBU SHIA ITHNAASHARIA....43

## Utangulizi

Sifa zote njema anastahiki Allaah Mola wa viumbe wote, na -Swala na Salamu zimfikie- Mtume Muhammad, aliyetumwa hali ya kuwa ni rehema kwa walimwengu wote, na pia ziwafikie, Jamaa zake na Maswahaba wake wote.

**Baada ya hayo:** Si jambo la siri kwa wanafunzi wenye kutafuta elimu ya kisheria, na wenye kujishughulisha na masuala ya kuwajibu Mashia, kwamba msimamo wa Shia Ithnaasharia dhidi ya watu wote wanaopinga nao, na kwamba wao Shia humkufurisha na kumtia katika upotevu kila anayepinga nao, bali huwakufurisha hata katika makundi mengine ya Kishia, kama vile Zaidiyyah, Ismailiyyah na makundi mengine ya Kishia. Huwazingatia wote hao ni makafiri na watu wa bidaa kwa mtazamo wa Shia Imaamiyah[(1)].

Shia Ithnaasharia wanajiona wao ndio kundi lenye kuokoka na lenye kunusuriwa, hilo wamelithibitisha wanazuoni wao, mfano: An-Naubakhtiy, Al-Qummiy, Al-Kasshiy na wengineo miongoni mwa maulamaa wa Shia Imaamiyyah.

**Swali:** Ni kwanini nimetunga risala maalumu kuhusu msimamo wa Shia Ithnaasharia dhidi ya Masufi?

**Jibu juu ya swali hili ni kuwa:** Watu wengi waliofanya Usufi kuwa ndio mfumo na njia yao katika kuadudu, hawaijui heshima na nafasi waliyonayo wao pamoja na wafuasi wao mbele ya Shia Imaamiyyah, na kabla sijaanza kueleza yale niliyonayo, nitawatajia baadhi ya vitabu wanachuoni wa kundi la Shia Imaamiyah katika kuwaema vibaya Masufi.

---

1 - Tazama Kitabu: [Shia Al-Immamiyyah Al-Ithnaasharia watakfiirihim li'umuumil muslimin] cha Abdullahi As-Salafi, na Kitabu: [Dhwaahiratu Ttakfiyr fiy Madh-habi Sshia'til Imaamiyyah Al-Ithnaashariyyah], Cha Dr. Abdur Rahman Ad-Dimashqiy, na Kitabu: [Al-Fikru Ttakfiyriy I'nda Sshia' Haqiyqatun Am-Iftiraa] Cha Mhakiki Abdul Malik As Shafi'y.

Anasema Al-hurru Al-a'miliy katika kitabu chake: [Risalatul Ithnaa A'shariyah fir- Raddi A'laas Suufiyah]: **"Katu hajawahi Shia yeyote kuwa Sufi, kama linavyo bainika hilo kwa wanaofuatilia vitabu vya hadithi, wapokezi na kusikia hadithi, bali haujatajwa Usufi na Wafuasi wake (Masufi) ndani ya vitabu vya Shia na maneno ya Maimam (alaihis salaam), isipokuwa hutajwa kwa vibaya, na hakika wametunga vitabu vingi katika kuwarudi Masufi, baadhi yake wamevitaja kwenye kitabu Fahris ya vitabu vya Shia"[2].**

Na ametaja Mhakiki wa kitabu hicho majina ya vitabu hivyo:

1. Ar Risaalatul Ithaasharia fir Raddi 'ulas Suufiyyah. Cha Al Hurrul 'Aamiliy.
2. Ar Raddu 'Alas Suufiyyah. Cha Mhakiki Al-Qummiy.
3. Ar Raddu 'Alas Suufiyyah. Cha Al-Maulaa Ismail bin Muhammad bin Hussein Al-Mazindraniy, maarufu kwa jina la Al-khawaajuiy.
4. Ar Raddu 'Alaas Suufiyyah. Cha As Sayyid A'dhwam Ali Bankuriy
5. Ar Raddu 'Alas Suufiyyah. Kimechukuliwa kutoka kwenye kitabu: [Hadiiqatus Shia] cha Al Ardabiiliy.
6. Ar Raddu 'Alas Suufiyyah. Kimeandikwa kwa lugha ya Kifursi katika zama za Fat-hi Ali Shah.
7. Ar Raddu 'Alas Suufiyyah. Kimeandikwa kwa lugha ya Kifursi na baadhi ya maulamaa wao.
8. Ar Raadu 'Alas Suufiyyah. Cha Amir Muhammad Taqi Al Kashmiriy.
9. Ar Raddu 'Alas Suufiyyah. Cha Mailaa Hassan bin Muhammad Ali Al Yazdiy.
10. Ar Raddu 'Alas Suufiyyah. Ali Al Majaaz bin Bahril 'uluum.
11. Ar Raddu 'Alas Suufiyyah. Cha Haji Muhammad Ridhwa Al Qazwiiniy,
12. Ar Raddu 'Alas Suufiyyah. Cha Muhammad Twahir An Najafi.
13. Ar Raddu 'Alas Suufiyyah. Cha Sheikh Muhammad Ali Mirza.

---

2- Tazama kitabu: [Ar Risaalatul Ithnaa A'shariyah fir Raddi A'laas Suufiyyah] (Uk. 12).

14. Ar Raddu 'Alas Suufiyyah. Cha Muhammad Ali Twabaatwabaiy.
15. Ar Raddu 'Alas Suufiyyah. Kimeandikwa Kifursi, cha Al Qadhi Al Haashimiy.
16. Ar Raddu 'Alas Suufiyyah. Cha sheikh Muhammad Ali Qatwifiy.
17. Ar Raddu 'Alas Suufiyyah. Cha Maulaa Mutwahar bin Muhammad, kimeandikwa kwa lugha ya Kifursi.
18. Ar Raddu 'Alas Suufiyyah. Kimeandikwa kwa lugha ya Kifursi, cha cha Maulaa Fat-hullaahi Al Mutakhallis.

Na vitabu vingine vilivyochapishwa na ambavyo bado havichapishwa (miswada)[3].

Na lengo langu kwenye risala hii ni kumzindua Sunni anayehitaji kuzinduka ili asirubuniwe na Taqiya ya Shia Imaamiyah na maneno yao matamu wanayosema kwenye minasaba mbalimbali ya kijamii na kwenye mikutano ya kuleta uhusiano na umoja, na katika minasaba mingineyo. Bali Masunni wanapaswa wawe na uelewa na maarifa ya kujua itikadi za hawa jamaa na yale yanayo adikwa ndani ya vitabu vyao.

Tena ni vyema wafuasi wa Twariqa za Kisufi wakafahamu kuwa; Shia wanawalaghai pale wanapodai kuwapenda, kuwaheshimu na kuwaiga Ahlil Bait, na kwamba mapenzi hayo waliyonayo wao (Masufi) kwa Ahlul Bait ni sawa na mapenzi ya Shia, kwa hiyo inapasa kushirikiana baina yao dhidi ya waislamu wengine.

Yote haya wanafanya Shia ili kuficha Taqiya ambayo inahudumu maslahi yao katika kueneza Ushia, na hilo linatokana na mpango wa Shia ulimwenguni unaolenga kuwaingiza Masunni kwenye Ushia, baada ya kukukumbana vikwazo vingi kutoka Masufi kwenye maeneo na nchi mbalimbali, ikawa miongoni mwa mambo ya wajibu katika Taqiya ni kuwalaghai Masufi, kujipendekeza kwao na kuficha msimamo wao dhidi ya Masufi.

3- Kitabu: [Ar Risaatul Ithnaa 'Asharia] (Uk. 13).

Na kupitia kitabu hiki itakubainikia wewe sababu zilizopelekea Shia kuwafanyia uadui Masufi na kuwakashifu, sababu kubwa ni msimamo Masufi kuhusu Qur'an Tukufu, Sunna za Mtume, Swahaba na Mama wa Waumini, mtazamo huu wa Masufi ni mtazamo wa haki ambao unaenziwa na kila anayejinasibisha na Uislamu na Sunnah, bali msimamo huu ndio umewafanya Shia Ithnaasharia kuwafanyia uadui Masufi na kuwapiga vita.

Kwa uwezo wa Allaah, risala hii itakuwa fupi kiasi cha kutaja riwaya mbalimbali za Maimamu wa Kishia katika kuwakufurisha masufi, kuwatia katika ujinga, na kuwaonya watu na Masufi, pasipo sisi kuingilia katika kufafanua au kukosoa, bali tutamuacha msomaji yeye mwenyewe atahukumu.

Na tutakapomtaja Sheikh yeyote wa Shia Imaamiyyuah, tutaweka utambulisho wake, na tutaeleza jinsi alivyosifiwa na wanachuoni wa Shia Imaamiyyah, na kubainisha nafasi yake ya kielimu (mbele ya Mashia), ili isije kusemwa kwamba sisi tunanukuu kutoka kwa watu wasiojulikana, au pakasemwa kwamba tunawasingizia Shia mambo wasiyoyasema wala kuitakidi.

Na mwanzo wa kitabu tutataja dibaji fupi mno, tutataja ndani baadhi ya itikadi za Shia Imaamiyyah ambazo zinatofautiana na itikadi za Masufi.

Hali ya kumuomba Allaah Mtukufu awanusuru Masunni, na aunganishe neno lao kwenye haki, na kufuata mwongozo wa Bwana wa Mitume Swala na Salamu zimshukie Yeye, Jamaa zake na Maswahaba-, na kila mwenye kufuata njia yao na mwenendo wao mpaka siku ya kiama.

**Ameandika**

**Abdallah ibn Mohammad**

**20/9/1435 Hijria**

## MAKOSA YA KIITIKADI KATI YA MASUFI NA SHIA IMAAMIYYAH

Hizi ni baadhi ya itikadi za Shia Imaamiyyah ambazo zinapingana na itikadi za Masufi, na haya ni mambo ya msingi wa dini, ambayo ni sababu inayopelekea kutowezekana kuungana wala kuleta umoja, jambo ambalo Mashia wanalidai, na wala hayatoi nafasi kwa mlinganizi kulingania watu katika umoja kati ya Shia Imaamiyyah na Masufi.

***********************************
***********************
***************

## MSIMAMO WA SHIA IMAAMIYYAH KUHUSU QUR'AN:
## (Kauli yao kwamba Qur'an imepotoshwa)[4]

Shia Imaamiyyah wanaamini kwamba Qur'an hii iliyopo mikononi mwetu imepotoshwa, na wametaja riwaya nyingi kuhusu jambo hilo:

- Kutoka kwa Hisham ibn Salim, kutoka kwa Abi Abdillah (alaihis salaam): **"Hakika Qur'an aliyokuja nayo Jibril (alaihis salaam) kwa Muhammad -Swala na Salamu zimshukie na Jamaa zake- ina aya Elfu kumi na saba"**[5].

Na ifahamike kwamba idadi ya aya zote za Qur'an ni tukufu ni aya (6236). Maana yake ni kwamba Qur'an wanayoidai Shia Raafidhwa ni mara tatu zaidi ya Qur'an iliyopo mikononi mwetu ambayo Allaah ameahidi kuilinda!!! Allaah atulinde.

---

4- Tazama kitabu: [Usuulu madh-habis Shiatil Imaamiyyah Al-Ithanai 'Ashariyyah] cha Dr. Nasir Al-Qifaari (Jz. 1, Uk. 125-303).

5- Tazama kitabu: [Usuul al-Kaafi] (Jz. 2, Uk. 634). Na riwaya hii imethibitishwa na Sheikh wao Al-Majlis, akasema katika kitabu chake: [Mir-aatul 'uquul] (Jz. 12, Uk. 525): **"Hadithi hii imethibitishwa"**, kisha akasema: **"Hadithi hii ni sahihi, wala hapana shaka yoyote kwamba hadithi hii na nyingine nyingi ni miongoni mwa hadithi zilizo wazi tena sahihi kuhusu kupunguzwa kwa Qur'an na kubadilishwa kwake, na msimamo wangu mimi ni kwamba maana ya hadihti hizi ni Mutawaatir"**. Hapadhaniwi katika hadithi hizi uwongo wowote.

- Na amesema Ni'matullaahi Al-jazaairiy: "**Hadithi zinazotaja kupotoshwa kwa Qur'an ni nyingi tena zipo wazi, (imebadilishwa) kimaneno, mada, na irabu yake"**[6]**.**
- Na amesema Al-Hurru Al-a'miliy: "Jua kwamba haki ambayo hakuna kuikwepa kwa mujibu wa hadithi zilizopokewa kwa wingi, ni kwamba: Qur'an hii tuliyonayo, ilikumbwa na mabadiliko baada ya kufa Mtume wa Allaah, na walioikusanya baada yake waliondosha maneno na aya nyingi...!! **Na mimi baada ya kufuatilia hadithi nyingi na kuchunguza athari mbalimbali nimeikubali ukweli wa kauli hii, kiasi ambacho inawezekana kusema, kuamini jambo hili ni katika misingi ya lazima katika madhehebu ya Kishia**"[7]**.**
- Na mwanachuoni wao An-Nuriy At-twabrasiy ametunga kitabu kinachothibitisha kubadilishwa kwa Qur'an amekiita**: [Faslul khitwaab fiy tahriyf Kitaabi Rabbil Arbaab]**, na ndani ya kitabu hiki ametaja maelezo mengi kuthibitisha kubadilishwa kwa Qur'an, na miongoni mwa dalili zake kuhusu kubadilishwa kwa Qur'an ni:
- Kutafautiana ufasaha wake wa hali ya juu kwenye baadhi ya vipengele ambavyo ni muujiza, na katika vipengele vingine kuna upuuzi (baadhi ya aya hazina maana), Allaah atukinge!! Na hapa akainukuu Sura inayoitwa -Surat al-wilayah- ambayo Mashia wanadai kwamba Maswahaba wameifuta ndani ya Kitabu cha Allaah (Qur'an).

Nayo ni: **"Enyi mlioamini ziaminini nuru mbili tulizoziteremsha, ambazo zinasomwa kwenu na zinawaonyeni na adhabu kubwa, nuru mbili baadhi yake zinatokana na baadhi nyingine, Nami ni Mwenye kusikia na Mjuzi mno. Hakika wale wanaotimiza (ahadi) na Mtume wake katika aya (za Allaah) watapata pepo zenye neema. Na wale waliokufuru baada ya kuamini kwa kuvunja ahadi yao na**

---

6- Rejea kitabu: [Al-Anwaaru Nnu'maaniyyah] (Jz. 2, Uk. 360-361).
7- Rejea kitabu: [Mir-aatul Anwaar] (Uk. 36).

**yale waliyo ahidiwa na Mtume watatupwa motoni, wamezidhulumu nafsi zao na wamemuasi Wasii wa Mtume, hao watanyweshwa maji ya moto”(8).**

Pia amesema: Ilisomwa aya hii mbele ya Abi Abdillaah:

﴿كُنتُمْ خَيْرَ أُمَّةٍ أُخْرِجَتْ لِلنَّاسِ﴾

**“Nyinyi mmekuwa umma bora waliyo tolewa watu”(9).**

Akasema Abu Abdillahi: **“Umma bora” na wanamuuwa Amiril Mu’miniin (Ally bin Abi Twalib), Hassan na Hussein -alaihimas salaam!!- Akauliza: Basi nitasomaje? Akasema: soma:**

كُنْتُمْ خَيْرَ ائِمَّةٍ

**“Mmekuwa nyinyi ni Maimamu bora”(10).**

Na kadhalika anasema katika Suratu al-inshiraah: Kutoka kwa Abu Abdillaah amesema: [Hivi ndivyo ilivyoteremka:

﴿أَلَمْ نَشْرَحْ لَكَ صَدْرَكَ ۝١ وَوَضَعْنَا عَنكَ وِزْرَكَ ۝٢ ٱلَّذِىٓ أَنقَضَ ظَهْرَكَ ۝٣ وَرَفَعْنَا لَكَ ذِكْرَكَ - بِعَلِيٍّ صِهْرَكَ -﴾

**“Kwani hatukikunjua kifua chako * Na tukakuondolea mzigo wako * Uliovunja mgongo wako * Na tukatukuza utajo wako kwa sababu ya Ally mkwe wako”(11).**

Hizi ndio baadhi ya sura zilizo badilishwa ambazo amezitaja na An Nuriy at- Twabrasiy, amezitaja sura zote za Qur'an na kile kilichopuzwa.

---

9- Surat Ali-Imran/110.

10- Kitabu: [Faslul Khitwaab] (Uk. 264).

11- Kitabu: [Faslul Khitwaab] (Uk. 268).

## ITIKADI YAO KUWA QUR'AN SI HOJA MPAKA AJE QAYYIM (MAHDI WAO)[12]

Haingii akilini kwa kundi linalodai kuwa ni waislamu, kisha wanaitakidi kwamba: (Qur'an si hoja)!. Hali ya kuwa Allaah anasema kumwambia yule anayetaka uthibitisho juu ya ukweli wa Mtume (Muhammad):

﴿أَوَلَمْ يَكْفِهِمْ أَنَّآ أَنزَلْنَا عَلَيْكَ ٱلْكِتَٰبَ يُتْلَىٰ عَلَيْهِمْ ۚ إِنَّ﴾

**"Kwani haikuwatosha washirikina hawa ili wajue ukweli wako, kuwa sisi tumekuteremshia Qur'an wanayo somewa?"[13].**

Qur'an Tukufu ni hoja na ni shahidi juu ya Utume wake.

Lakini Sheikh wa Kishia Al-Kulein, ambaye wanamuita "Thiqatul Islaam" anapokea riwaya ndani ya kitabu chake: [Usuulul Kaafi", inasema: **"Qur'an haiwezi ikawa ni hoja mpaka kwa kupatikana Qayyim. Na kwamba Ally ndiye aliyekuwa Qayyim wa Qur'an, na kumtii yeye ni faradhi, na alikuwa ni hoja kwa watu baada ya kufariki Mtume"[14].**

Maana ya maneno haya ni kuwa kauli ya Imamu mbele ya mashie ni bora na fasaha zaidi kuliko maneno ya Allaah (Qur'an), na kwa sababu hii wamekiita Kitabu cha Allaah kuwa ni: **Qur'an iliyo nyamaza**, na wakamwita Imamu wao kuwa ni: **Qur'an inayoongea**. Na wanadai kwamba wamepokea kutoka kwa Ally kuwa amesema**: "Hiki ni kitabu cha Allaah kilicho nyamaza, Na mimi ni Kitabu cha Allaah kinachoongea"[15]**. Na wakati mwingine wadai kuwa Maimamu kumi na mbili ndio Qur'an yenyewe, ndio maana wanatafsiri kauli ya Allaah:

﴿وَٱتَّبَعُوا۟ ٱلنُّورَ ٱلَّذِىٓ أُنزِلَ مَعَهُۥٓ﴾

**"Na wakaifuata nuru iliyoteremshwa pamoja naye". [Al-A'raaf/157].**

Wanasema: Nuru hapo ni Maimamu -alaihimus salaam-.

---

12- Faida hii ipo ndani ya kitabu: [Usuul madh-habi Shiia al-Imaamiyya] (Jz. 1, Uk. 127-132).
13- Surat Al-'Ankabut/51.
14- Kitabu: [Usuul Kaafi] (Jz. 1, Uk. 188).
15- Kitabu: [Al-Fusuulul muhimma] cha Al-Hurrul 'Aamiliy (Uk. 235).

## ITIKADI YAO KWAMBA MAIMAMU NDIO WAJUZI ZAIDI WA QUR'AN KULIKO MTU YEYOTE

Imekuja hadithi ndefu kwenye Kitabu: [Usuulul Kaafi], kutoka kwa Abu Abdillaahi amesema: **"Hakika watu inawatosha wao Qur'an lau wakimpata wa kuitafsiri, na Mtume -Swala na Salamu zimshukie- tayari aliitafsiri Qur'an yote kwa mtu mmoja tu, ambaye ni Ally Bin Abi Twalib, naye ndiye mwenye jukumu la kuitafsiri kwa umma"[16].**

Na imepokewa kutoka kwa Abu Ja'far: **"…Hakika ni wajibu kwa watu kuisoma Qur'an kama ilivyo teremshwa, na iwapo watahitaji tafsiri yake, basi warudi kwetu na sisi ndio wenye mwongozo wake"[17].**

## KAULI YAO KWAMBA SEHEMU KUBWA YA QUR'AN IMETEREMKA KWAO NA KWA MAADUI ZAO

Shia wanasema wakinukuu kutoka kwa Maimamu wao kwamba: **"Sehemu kubwa ya Qur'an imeteremka kwao (Maimamu 12), kwa wapenzi wao na maadui zao"[18].** Pamoja na hayo, lau utafanya utafiti kwenye Kitabu cha Allaah (Qur'an), ukachukua na Kamusi zote za lugha ya Kiarabu, ukatafuta jina moja miongoni mwa majina ya Maimamu hawa kumi na mbili, katu hutokuta utajo wao!! Lakini pamoja na hivyo, Sheikh wao Al-Baharaniy amedai kwamba Ally pekee ametajwa ndani ya Qur'an mara (1154), na akaandika kitabu kuhusu jambo hili na kukiita: **[Al-Lawaamiu Nnuuraniyyah fii Asmaai Alliy Wa-ahli baytihil Qur'aaniyyah],** amepinga ndani yake Kamusi zote za kiarabu na amekiuka misingi ya akili na falsafa.

- Na baadhi ya riwaya zao zinasema: **[Qur'an imeshuka katika robo nne: Robo moja imeshuka kwetu, robo ya pili kwa maadui zetu, robo ya tatu ni Sunnah na mifano, na robo ya nne ni hukumu na mirathi][19].**

---

16- Kitabu: [Usuul al-Kaafi] (Jz. 1, Uk. 25) na [Wasaailu Sshiia] (Jz. 18, Uk. 131).
17- Kitabu: [Wasaailu Sshiia] cha Al-Hurrul 'Aamiliy (Jz. 27, Uk. 202).
18- Kitabu: [Tafsiiru Sswaafi] (Jz. 1, Uk. 24).
19- Kitabu: [Usuulul Kaafi] (Jz. 2, Uk. 627) na [Al-Burhan] (Jz. 1, Uk. 21).

- Na katika riwaya nyingine kutoka kwa Amiril mu'miniin -alaihis salaam: **[Qur'an imeteremka katika robo nne: Robo moja imeshuka kwetu, robo ya pili imeshuka kwa maadui zetu, robo ya tatu ni Sunnah na mifano, na robo ya nne ni mirathi na hukumu mbalimbali za dini. Lakini Qur'an halisi ipo kwetu sisi]**[20]
- Na katika riwaya nyingine kutoka kwa Amiirul Mu'miniin -alaihis salaam-: **[Qur'an imeshuka katika theluthi tatu: Theluthi moja kwetu sisi, theluthi ya pili ni Sunnah na mifano, na theluthi ya tatu ni mirathi na hukumu mbalimbali]**[21].

## MSIMAMO WA SHIA IMAAMIYYAH KUHUSU SUNNAH (HADITHI) ZA MTUME -SWALA NA SALAMU ZIMSHUKIE-

Sunna za Mtume huzingatiwa ni chanzo cha pili cha sheria za kiislamu baada ya Qur'an Tukufu, nazo ni sehemu ya Wahyi ambao Allaah ameuhusisha kwa Mtume wake -Swala na Salamu zimshukie-, Mtume wa Allaah hazungumzi kwa utashi wake, na kwa sababu hiyo, kutii, kunyenyekea na kusalimu amri kwenye madhumuni ya Sunnah, ndio muktadha wa kushuhudia kwamba Muhammad ni Mjumbe wa Allaah -Swala na na Salamu zimshukie-, Mjumbe kutoka kwa Mfalme wa walimwengu wote, na ndiye aliye na jukumu la kuifikisha dini kwa watu wote. Allah anasema:

﴿فَلْيَحْذَرِ الَّذِينَ يُخَالِفُونَ عَنْ أَمْرِهِ أَن تُصِيبَهُمْ فِتْنَةٌ أَوْ يُصِيبَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ﴾

**"Basi wajihadhari wale wanaokaidi amri yake, Usije ukawapata msiba au ikawafika adhabu chungu"**[22].

Na pia amesema:

﴿فَلَا وَرَبِّكَ لَا يُؤْمِنُونَ حَتَّىٰ يُحَكِّمُوكَ فِيمَا شَجَرَ بَيْنَهُمْ ثُمَّ لَا يَجِدُوا فِي أَنفُسِهِمْ حَرَجًا مِّمَّا قَضَيْتَ وَيُسَلِّمُوا تَسْلِيمًا﴾

---

20- Kitabu: [Bihaarul Anwaar] (Jz. 24, Uk. 306).
21- Kitabu: [Usuul al-Kaafi] (Jz. 2, Uk. 628).
22- Surat An-Nuur/63.

**“Naapa kwa Mola wako Mlezi, Hawatakuwa waumini (wa kweli) mpaka wakufanye wewe ndiye muamuzi katika yale wanayo khitilafiana, kisha wasione uzito katika nyoyo zao juu ya hukumu uliyotoa, na wanyenyekee kabi”a”**[23].

Na Mtume -Swala na Salamu zimshukie- amesema: **“Nisimkute kabisa mmoja wenu amekaa kwenye kiti chake, inamjia yeye hadithi miongoni mwa hadithi zangu, (inataja jambo ambalo) nimeamrishwa au kukatazwa, kisha anasema: Sisi hatulijui. Sisi tutafuata lile tulichokipata katika Qur’an”**[24].

Na Imam Shafi'i -Allaah amrehemu- anasema: **“Sijamsikia mtu yeyote aliyenasibishiwa elimu au kujinasibishia yeye mwenyewe elimu, anaepinga kwamba (Allaah) amewajibisha kufuata amri ya Mtume -Swala na Salamu zimshukie-, na kujisalimisha kwenye hukumu yake, kwa sababu Ta’alaa hakumjaalia mtu yeyote aliyekuja baada yake isipokuwa ni kumfuata Yeye, na kwamba kauli yoyote si lazima kuifanyia kazi, isipokuwa kwa ushahidi wa Qur’an au Sunna za Mtume wa Allaah -Swala na Salamu zimshukie-, na kwamba kisichokuwa viwili hivyo ni lazima kufuata viwili hivyo (Qur’an na Sunnah), na kwamba amefaradhisha juu yetu sisi, waliokuwa kabla yetu, na watakaokuja baada yetu, ni kuzikubali hadithi za Mtume -Swala na Salamu zimshukie-, hakuna anayepinga kwamba ni wajibu kuzikubali hadithi kutoka kwa Mtume -Swala na Salamu zimshukie-”**[25].

Ama mashia wao wamezitupa Sunnah hizo nyuma ya migongo yao, na wahawakuipa uzito amri yoyote ya Allaah iliyokuja kupitia hadithi za Mtume wake, na badala yake wamekuja na ufafanuzi na kuelezea maana ya Sunnah bila ya hoja yoyote, wala maana hiyo haitambuliki na watu wa mwanzo waliotangulia.

---

23- Surat An-Nisaa/65.
24- Kitabu: [Abu Daud] (4605), [Tirmidh] (2663) na [Ibn Majah] (13)
25- Kitabu: [Al-Ummu] (Jz. 7, Uk. 287).

Maana ya Sunnah mbele ya mashia ni: **[Kila kauli ya Imam (ma'asuum), kitendo chake, au jambo lililofanywa mbele yake akalinyamazia]**[26]**.**

Na Ma'asuum (aliyekingwa na kutenda dhambi) mbele ya mashia ni: Mtume Muhammad na Maimamu wao kumi na mbili.

Hii ndiyo daraja waliyowapa Maimamu wao, ni wajibu kuwatii na kuwafuata kama linavyopasa hilo kwa Mtume wetu Muhammad -Swala na Salamu zimshukie-. Wala hakuna tafauti kati ya kauli aliyoisema Imamu wao na kauli aliyoisema Mtume ambaye hazungumzi kwa matashi yake isipokuwa kwa wahyi aliyopewa.

Na kwa msingi huo ndio mmoja wa Masheikh wao wa zama hizi Abdullaah Fayyadh: **[Hakika kuamini kutokosea kwa Maimamu, ndio kumefanya hadithi zilizokiuja kutoka kwao ni sahihi, bila kuweka sharti la kuungana kwa sanadi ya wapokezi wake mpaka kwa Mtume, kama linavyofahamika kwa Ahlul Sunnah]**[27]**.** Hayo ni kwa sababu mashia wanaamini kwamba Uimamu ni mwendelezo wa Utume, kama alivyosema wazi hilo sheikh wao Muhammad Ridhwaa Al-Mudhwaffar[28].

Ama Ibn Baabawayhi Al-Qummi yeye amesema wazi kwamba Maimamu ni sawa na Manabii, amesema: **[Kauli yao ni sawa na kauli ya Allaah, na amri yao ni saw ana amri ya Allaah. Na kuwatii wao ni kumtii Allaah, na kuwaasi wao ni kumuasi Allaah. Na hawatamki lolote isipokuwa kwa wahyi kutoka kwa Allaah]**[29]**.**

Na kupitia itikadi hii, Shia wamesema uongo mwingi kupitia ndimi za Maimamu wao kwa madai kwamba wao ndio waliyo waamrishwa kufanya hivyo. Imepokewa hadithi katika kitabu Al-Kaafi: Kutoka kwa Abu Abdillaah, amesema: **[Simulizi yangu ni simulizi ya baba yangu, na**

---

26- Kitabu: [Al-Usuulul 'Aamah lil-fiqhil muqaaran] cha Muhammad Taqi Al-Hakim (Uk. 122).
27- Kitabu: [Taareikh al-Imaamiyyah] cha Abdullaah Fayyadh (Uk. 140).
28- Kitabu: ['Aqaaid al-Imaamiyyah] cha Muhammad Ridhwaa Mudhaffar (Uk. 166).
29- Kitabu: [Al-I'tiqadaat] (Uk. 106)

**simulizi ya baba yangu ni simulizi ya babu yangu, na simulizi ya babu yangu ni simulizi ya babu Husein, na simulizi ya Hussein ni simulizi ya Hassan, na simulizi ya Hassan ni simulizi ya Amirul Mu'uminina, na simulizi ya Amirul Muuminina ni simulizi ya Mtume wa Allaah, na simulizi ya Mtume wa Allaah ni kauli ya Allaah][30].**

Na mshereheshaji wa kitabu (Al-kaafi) ameeleza kwamba kauli hiyo inajuilisha kuwa; **[Hadithi yoyote iliyosimuliwa kutoka kwa Imamu Mtwaharifu hiyo ni kauli ya Allaah Ta'alaa, wala hakuna mgongano kwenye kauli zao, kama ambavyo hakuna mgongano kwenye kauli za Allaah Ta'alaa][31].** Lakini tukirudi kwenye vitabu vya Aqida na Fiqhi vya mashia, tunapata kwamba mashia wameenda kinyume na itikadi yao hii potofu, nayo ni kulingana sawa Manabii na Maimamu katika kufikisha ujumbe, na wajibu wa kutiiwa, bali utapata hupati ndani ya vitabu vyao amri yoyote wala katazo isipokuwa kutoka kwa Maimamu, na Mtume -Swala na Salamu zimshukie- hana nafasi yoyote, na hadithi kutoka kwa Maimamu ni nyingi kuliko hadithi kutoka kwa Mtume.

Je, watu hawa wanaamini kweli uwepo wa Mtume Muhammad -Swala na Salamu zimshukie- na kuamini risala yake! Hapana…

## MSIMAMO WA SHIA IMAAMIYAH KUHUSU MASWAHABA WA MTUME -SWALA NA SALAMU ZIMSHUKIE-

Maswahaba watukufu wana daraja kubwa na cheo kikubwa mbele ya waislamu, wao ni viumbe bora baada ya Mitume na Manabii, na watwaharifu zaidi wa nyoyo. Allaah amewateua wao ili kusuhubiana na Mtume wa mwisho na Mjumbe wa Mola wa viumbe wote, na ni vigumu kuja baada yao watu walio bora zaidi kuliko wao. Hilo ni kwa ushahidi wa bwana wa viumbe Mtume wetu Muhammad -Swala na Salamu

30- Kitabu: [Usuul al-Kaafi] (Jz. 1, Uk. 53), na [Wasaailu Sshii'a] (Jz. 18, Uk. 58).
31- Kitabu: [Sharh Jaami' 'alal Kaafi] cha Al-Maazindraani (Jz. 2, Uk. 272)

zimshukie-, pale aliposema: **"Watu bora ni wa karne yangu kisha wanaofuatia hao kisha wanaowafuatia"**[32].

Na kwa nini isiwe hivyo, hali ya kuwa Allaah amewatakasa wao kutokea juu ya mbingu sab,a Allaah Ta'alaa anasema:

﴿وَٱلسَّٰبِقُونَ ٱلْأَوَّلُونَ مِنَ ٱلْمُهَٰجِرِينَ وَٱلْأَنصَارِ وَٱلَّذِينَ ٱتَّبَعُوهُم بِإِحْسَٰنٍ رَّضِيَ ٱللَّهُ عَنْهُمْ وَرَضُوا۟ عَنْهُ وَأَعَدَّ لَهُمْ جَنَّٰتٍ تَجْرِى تَحْتَهَا ٱلْأَنْهَٰرُ خَٰلِدِينَ فِيهَآ أَبَدًا ۚ ذَٰلِكَ ٱلْفَوْزُ ٱلْعَظِيمُ﴾

**"Na wale waliotangulia wamwanzo miongoni mwa Muhajirina na Answari, na wale waliowafuata wao kwa wema, Allaah ameridhika nao wao wataridhika naye, na awmewaandalia wao Mabutsani ipitayo mito chini yake, hali ya kukaa humo milele. Huku ndiko kufuzu kukubwa"**[33].

Na Allaah anasema:

﴿مُّحَمَّدٌ رَّسُولُ ٱللَّهِ ۚ وَٱلَّذِينَ مَعَهُۥٓ أَشِدَّآءُ عَلَى ٱلْكُفَّارِ رُحَمَآءُ بَيْنَهُمْ ۖ تَرَىٰهُمْ رُكَّعًا سُجَّدًا يَبْتَغُونَ فَضْلًا مِّنَ ٱللَّهِ وَرِضْوَٰنًا ۖ سِيمَاهُمْ فِى وُجُوهِهِم مِّنْ أَثَرِ ٱلسُّجُودِ ۚ ذَٰلِكَ مَثَلُهُمْ فِى ٱلتَّوْرَىٰةِ ۚ وَمَثَلُهُمْ فِى ٱلْإِنجِيلِ كَزَرْعٍ أَخْرَجَ شَطْـَٔهُۥ فَـَٔازَرَهُۥ فَٱسْتَغْلَظَ فَٱسْتَوَىٰ عَلَىٰ سُوقِهِۦ يُعْجِبُ ٱلزُّرَّاعَ لِيَغِيظَ بِهِمُ ٱلْكُفَّارَ ۗ وَعَدَ ٱللَّهُ ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ وَعَمِلُوا۟ ٱلصَّٰلِحَٰتِ مِنْهُم مَّغْفِرَةً وَأَجْرًا عَظِيمًۢا﴾

**"Muhammad ni Mtume wa Allah. Na walio pamoja naye ni wenye nyoyo thabiti mbele ya makafiri na wenye kuhurumiana wao kwa wao. Utawaona wakiinama kwa kurukuu na kusujudu, wakitafuta fadhila za Allah na radhi zake. Alama zao zi katika nyuso zao, kwa athari ya kusujudu. Huu ndio wasifu katika Taurati. Na wasifu wao katika Injili ni kama mmea uliotoa chipukizi lake, kisha ukalitia nguvu, ukawa mnene, ukasimama sawasawa juu ya ubuwa wake, ukawafurahisha wakulima, ili kuwakasirisha kwa ajili yao makafiri. Allaah amewaahidi walio amini na wakataenda mema katika wao msamaha na ujira mkubwa"**[34].

---

32- Kitabu: [Bukhari] (2652) na [Muslim] (2533).
33- Surat At-Tauba/100.
34- Surat Al-Fat'h/29.

Na Allah anasema:

﴿لَّقَدْ رَضِيَ ٱللَّهُ عَنِ ٱلْمُؤْمِنِينَ إِذْ يُبَايِعُونَكَ تَحْتَ ٱلشَّجَرَةِ فَعَلِمَ مَا فِي قُلُوبِهِمْ فَأَنزَلَ ٱلسَّكِينَةَ عَلَيْهِمْ وَأَثَٰبَهُمْ فَتْحًا قَرِيبًا﴾

**"Kwa hakika Allaah amewaridhia Waumini walipokupa wewe mkono wa ahadi chini ya mti, Allaah alijua yaliyomo nyoyoni mwao. Basi akateremsha utulivu juu yao, na akawapa ushindi wa karibu (amba oni kuiteka Khaybar)"[35].**

Na Imam At-Twahawiy -Allaah amrehemu- anasema: **"Na tunawapenda maswahaba wa Mtume wa Allaah, wala hatuchupi mipaka kwenye kumpenda zaidi mmoja wao (kuliko mwingine), na wala hatujitengi na yeyote kati yao, na tunamchukia yule anayewachukia hao, na (tunamchukia) yule anayewataja kwa ubaya, na wala hatuwataji isipokuwa kwa wema. Na kuwapenda wao ni Dini, Imani na Ihsani (Kutenda wema), na kuwachukia ni kufuru, unafiki na kuvupa mipaka"[36].**

Ama itikadi ya Shia Raafidhwa imejikita katika kuwatukana, kuwashutumu na kuwakufurisha maswahaba -Allaah awaridhie-, na kumkufurisha kila anayewapenda wao na kuwatawalisha.

Imekuja katika kitabu: (Al-Kaafi): Kutoka kwa Hanaan, kutoka kwa baba yake, kutoka kwa Ja'far (a.s) amesema: **[Watu wote waliritadi (wakatoka kuucha uislamu), baada ya kufariki Mtume -Swala na Salamu zimshukie- isipokuwa watu watatu, nikauliza: Ni akina nani hao watatu? Akasema: Mikidadi Ibnul As'wad, Abu Dharri Al-Ghifary, na Salmaan Al-Faarisiy][37].**

Na Al-Majlisi ametaja kwenye kitabu: (Bihaarul An-waar): **[Kwamba Mahuri (mtumwa aliyeachwa huru) na Ali ibnil Hussein amesema: "Nilikuwa pamoja naye (Ali ibnil Hussein) kwenye baadhi ya faragha**

35- Surat Al-Fat'h/18.

36- Kitabu: [Sharh aqiida Ttwahaawiyyah] (Jz. 2, Uk. 689).

37- Kitabu: [Al-Kaafi] (Jz. 8, Uk. 245).

**zake, nikasema: Mimi nina haki kwako (lazima) uniambie kuhusu watu hawa wawili: Abubakar na Omar? Akasema: Hao ni makafiri, na ni kafiri yule atakayewapenda hao!"].**

Na imepokewa kutoka kwa Abu Hamza At-Thamaaliy, kuwa Yeye alimuuliza Ally ibnu Hussein kuhusu watu hao wawili (Abubakar na Omar) Akasema: **[Hao ni makafiri na ni kafiri yule atayewapenda]**[38].

Na katika tafsiri ya Al-Qummi kwenye kauli yake Allaah:

﴿إِنَّ ٱللَّهَ يَأۡمُرُ بِٱلۡعَدۡلِ وَٱلۡإِحۡسَٰنِ وَإِيتَآيِٕ ذِي ٱلۡقُرۡبَىٰ وَيَنۡهَىٰ عَنِ ٱلۡفَحۡشَآءِ وَٱلۡمُنكَرِ وَٱلۡبَغۡيِۚ﴾

**"Hakika Alllah anaamrisha kufanya uadilifu, na hisani, na kuwapa jamaa (ndugu wa karibu). Na anakataza uchafu, uovu, na dhulma"**[39].

Wamesema shia wakati wakifafanua aya hii: **[Uchafu ni Abubakar, Uovu ni Omar, na dhulma ni Othman]**[40].

Na Al-Majlisiy katika kitabu chake amezitaja riwaya nyingi za hadithi zinzosema: **[kwamba Abubakar, Omar, Othman, na Muawiyah, hao wamo ndani ya masanduku ya moto, Allaah atukinge]**[41].

Isitoshe mashia wamejaalia mahali pa kukidhi haja, ni miongoni mwa sehemu takatifu zaidi za kuwalaani maswahaba -Allaah awaridhie-.

Anasema sheikh wao Muhammad At-Tuweisirkani (wanamuita: 'Umdatul 'Ulamaa wal-Muhaqqiqiin): **[Jua, kuwa sehemu tukufu zaidi, na wakati bora na mazingira mazuri kuliko yote, katika kuwalaani -Allaah awalaani- pale unapokuwa chooni, utasema kwa kukariri kila unakidhi haja ndogo na kubwa, na wakati wa kujisafisha: "Ewe Mola mlaani Omar, kisha Abubakar na Omar, kisha Othman na Omar, kisha Muawiyah na Omar, kisha Yazid na Omar, kisha Ibn Ziyad na Omar, kisha Ibn Sa'ad na Omar, kisha Shimru na Omar, kisha askari wao na**

38- Kitabu: [Bihaar al-Anwaar] (Jz. 69, Uk. 137-138).
39- Surat [An-Nahli/90].
40- Kitabu: [Tafsiir Al-qummi] (Jz. 1, Uk. 390).
41- Kitabu: [Biharu Al-anwaar] (30, Uk. 399):

**Omar. Ewe Allaah mlaani Aisha, Hafsa, Hindu na Ummul Hakam, na mlaani kila anayeridhia vitendo vyao mpaka siku ya kiyama"]**[42]**.**

Maneno haya yanabaisha wazi chuki yao iliyojificha dhidi ya maswahaba wema, mpaka wanaona kwamba sehemu ya najisi (chooni), ni mahali patukufu pa kuwalaani maswahaba, na wakachagua wakati wa kukidhi haja ndio wakati bora zaidi wa kuwaombea wao laana. Je kuna dini yoyote unayoijua, inawaamrisha wafuasi wao kuwatukana maiti, na kujihisi unapata raha kwa kuwalaani wao hata wakati wa kukidhi haja!!.

## MSIMAMO WA SHIA DHIDI YA MAMA WA WAUMINI (WAKEZE MTUME -SWALA NA SALAMU ZIMSHUKIE-)

Itikadi ya shia imejikita juu ya kuwachukia na kuwafanyia uadui Mama wa waumini (wakeze Mtume -Allaah awaridhie-), na hasa Aisha na baba yake, ambaye ni Abubakar Swidiq -Allaah amridhie-, na Hafsa na baba yake, ambaye ni Omar ibn Al-khattwab -Allaah amridhie- Al-Farouq.

Anasema Sheikh wao Al-Majlisi: **[Na itikadi yetu katika kujitenga, sisi tunajitenga na masanamu manne Abubakar, Omar, Othman na Mu'awiyah. Na tunajitenga na wanawake wanne Aisha, Hafswa, Hindu na Ummul Hakam, na wafuasi na watetezi wao wote, na kwamba wao ni waovu zaidi katika ardhi hii kuliko viumbe wote wa Allaah, na kwamba haitimii imani ya kumuamini Allaah na Mtume wake na Maimamu isipokuwa baada ya kujitenga na maadui zao !]**[43]**.**

Na miongoni mwa chuki zao zilizojificha kwa Mama wa waumini, ni kumtuhumu kwao Aisha na Hafswa kuwa ndio waliyomuua Mtume -Swala na Salamu zimshukie-.

Amepokea sheikh wao Al-'ayyash kwa sanadi yake mpaka kwa Abu Abdillaahi Ja'far As-swadiq kuwa alisema: **[Hivi mnajua, Mtume amekufa mwenyewe au ameuwawa?]. Hakika Allaah anasema:**

42- Kitabu: [Laaliy al-Akhbaar] (Jz. 4, Uk. 92).

43- Kitabu: [Haqqul yaqiin] cha Muhammad Baqir Al-Majlis (Uk. 519).

﴿أَفَإِيْن مَّاتَ أَوْ قُتِلَ ٱنقَلَبْتُمْ عَلَىٰٓ أَعْقَٰبِكُمْ﴾

**"Je, akifa au akiuwawa ndiyo mtarudi nyuma (mkaacha dini na kuwa makafiri?"[44].**

**Mtume alipewa sumu kabla ya kufa, hao wawili (Hafsa na Aisha) ndiyo walio mnywesha sumu kabla ya kufariki[45], tukasema: Hao wawili na baba zao ni viumbe waovu zaidi katika viumbe vya Allaah][46].**

Na Al-majlisi ameitaja sanadi ya riwaya hii, na akasema ni riwaya inayozingatiwa, na akaitolea ufafanuzi akasema: **[Hakika Al-ayyaash amepokea kwa sanadi inayozingatiwa, kutoka kwa As-swadiq -alais salaam-: "Kwamba Aisha na Hafswa laana ya Allaah iwashukie wao na baba zao, ndio waliomuua Mtume wa Allaah kwa njama ya kumnywesha sumu"][47].**

Na miongoni mwa chuki zao dhidi ya Aisha na Hafwa -Allaah awaridhie, ni madai yao kwamba Allaah amepiga mfano wa mke wa Nuh na mke wa Luti kwa Aisha na Hafswa -Allaah awaridhie-

﴿ضَرَبَ ٱللَّهُ مَثَلًا لِّلَّذِينَ كَفَرُوا۟ ٱمْرَأَتَ نُوحٍ وَٱمْرَأَتَ لُوطٍ ۖ كَانَتَا تَحْتَ عَبْدَيْنِ مِنْ عِبَادِنَا صَٰلِحَيْنِ فَخَانَتَاهُمَا فَلَمْ يُغْنِيَا عَنْهُمَا مِنَ ٱللَّهِ شَيْـًٔا وَقِيلَ ٱدْخُلَا ٱلنَّارَ مَعَ ٱلدَّٰخِلِينَ﴾

**"Allaah amewapigia mfano wa waliokufuru: Mke wa Nuhu na Mke wa Luti. Walikuwa chini ya ndoa ya waja wetu wawili walio wema, lakini wakawafanyia khiyana (waume zao Nuh na Luti), nao hawakufaa kitu kuwaepusha na adhabu ya Allaah. Na wakaambiwa: "Ingieni Motoni pamoja na wanaoingia !"[48].**

Anasema Sheikh wao Al-faydhul Kaashaniy wakati anaitafsiri aya hii: **[Allaah amepiga mfano wa hali ya makafiri na wanafiki, kwamba wao**

44- Surat Aal-'Imraan/144.
45- Kitabu: [Tafsiir As-swaafi] (Jz. 1, Uk. 305). Na amezidisha Al-kaashani: **"Anakusudia wanawake wawili, ambao Allaah amewalaani wao na baba zao**"]
46- Kitabu: [Tafsiirul 'ayyaash] (Jz. 1, Uk. 200), [Tafsiirus Swaafi] ya Al-kashaani (Jz. 1, Uk. 305)
47- Kitabu: [Hayaatul Quluub] cha Al-majlis (Jz. 2, Uk. 700).
48- Surat At-tahrim/10.

**wataadhibiwa kwa sababu ya kufuru na unafiki wao, wala hautazingatiwa ukaribu wa mafungamano na nasaba uliyopo baina yao na Mtume -Swala na Salamu zimshukie-, (amepiga mfano) kwa hali ya mke wa Nabii Nuh na Nabii Luti. Hapa pana fumbo kwa Aisha na Hafsa kwa khiyana yao waliomfanyia Mtume -Swala na Salamu zimshukie- na kueneza siri yake na unafiki wao kwake, na kumpinga kwao, kama walivyofanya wake hao wawili wa Mitume hao, wala hawakuwasaidia kitu kuwaepusha na adhabu ya Allaah]**(49)**.**

Amesema Al-majlisi wakati anaifafanua aya hii: **[Wala haifichiki kwa mkosoaji huyu Mjuzi, Aliye makini, na Mwerevu, fumbo lililotajwa katika aya hizi, na kutajwa wazi unafiki wa Aisha na Hafsa na ukafiri wao]**(50)**.**

Kama ambavyo haikusalimika heshima ya Mama wa waumini Aliye twahara, na amemtakasa Allaah kutoka juu ya mbingu saba, shia (Raafidhwa) wamemtuhumu Aisha kwa uzinifu, -Allaah atukinge-, Hapana shaka huku ni kumkadhibisha Allaah ambaye ameteremsha aya nyingi katika kumtakasa Aisha, ambazo zinasomwa mkapa siku ya kiama, pia ni kumtusi Mtume wa Allaah -Swala na Salamu zimshukie-.

Ametaja sheikh wao Rajab Al-barsi kwamba: **[Aisha alikusanya pesa dinari Elfu arobaini kwa njia ya khiyana (uzinifu), na kuzigawa kwa watu wanaomchukia Ally]**(51). Bali wamemfanya mke wa Mtume -Swala na Salamu zimshukie- ni mhamasishaji wa uzinzi na ukahaba.

Ametaja sheikh wao At-twabrasi kwenye kitabu chake (Al-ihtijaaj): **[Kwamba siku moja Aisha alimpamba msichana aliyekuwa anaishi nyumbani kwake, akamwambia: Huenda tukamnasa kupitia msichana huyu kijana miongoni mwa vijana wa Ki-kureishi atakayempenda"**(52)**.**

49- Kitabu: [Tafsiir As-swaafi] (Jz. 2, Uk. 720).
50- Kitabu: [Bihaaru al-Anwaar] (Jz. 22, Uk. 33).
51- Kitabu: [Mashaariqu Anwaaril yaqiin] cha Rajab Al-barsi (Uk. 86).
52- Kitabu: [Al-ihtijaaj] (Uk. 82). Huu ni mukhtasari juu ya msimamo wa Shia Imaamiyyah dhidi ya Qur'an, Sunnah, Maswahaba na Mama wa Waumini. Na atayetaka ziada arejee vitabu

## DUA YA KUWALAANI MASANAMU MAWILI YA KIKUREISH
**(Wanamkusudia Abu Bakri, Omar, Aisha na Hafsa -Allah awaridhie)-.**

Imekuja ndani yake dua hiyo: **[Kwa jina la Allaah, Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu, "Ewe Allaah, mrehemu Muhammad na jamaa wa Muhammad. Ewe Allaah, teremsha laana yako kwa masanamu mawili ya Kikureishi na mashetani yao, na waongo wao (anakusudia: Abubakar na Omar), pamoja na binti zao wawili (Aisha na hafsa), ambao wamekhalifu amri zako, wakakanusha wahyi wako, wakapinga fadhila zako, wakabadilisha dini yako, na kukipotosha kitabu chako (Qur'an)… Ewe Allaah, walaani wao, wafuasi wao, marafiki zao, jamaa zao na vipenzi vyao… Ewe Allaah, walaani wao wakiwa kwenye siri zao na dhahiri yao, laana yenye kuendelea na kudumu… kisha soma mara nne: Ewe Allaah, waadhibu wao adhabu ambayo watu wa motoni wanaomba waepushwe nayo. Aamin, ewe Mola wa viumbe"[53].**

Kama ambavyo mashia wanafurahi na kusherehekea siku aliyouwawa Al-faruoq Omar ibnil Khatwab -Allaah amridhie- na wanamuita yule aliyemuua Abu Lu'ului Al-majuusiy (mwabudu moto), kwa jina la Baba shujaa'i Ddiyn[54].

---

vya sheikh Abdullah As-salafi -Allaah amhifadhi-, na kitabu: [Majmuu' muallafaat As-shaikh Muhammad Maalullaah…] kitabu hiki amekipangilia sheikh Ally bin Abdillaah Al-ammari.
53- Kitabu: [Ihqaaqul haqqi waidh-haaqul baatwil] cha Qadhi Nourullaah Al-mar'ashiy (Jz. 1, Uk. 137-178).
54- Kitabu: [Abbas Al-qummi], [Al-kunaa wal-alqaab] (Jz. 2, Uk. 55).

# MSIMAMO WA SHIA IMAAMIYYAH ITH-NAASHARIA DHIDI YA MASUFI

## MASUFI MBELE YA SHIA IMAAMIYYAH NI WATU WAOVU, WAMELAANIWA, NA KUFUKUZWA KATIKA REHMA ZA ALLAH

Anasema Al-hurrul 'Aamiliy[55] katika utangulizi wa kitabu chake: **[Wakati nilipoona mashia wengi dhaifu wameacha njia ya wakongwe wao, na maimamu wao katika kufuata hukumu za sheria, na wakafuata njia za maadui zao, ambao wanafanya Istihzai na kuacha kurejea kwao (maimamu) katika kuchukua hukumu mbalimbali za dini, na badala yake wakazusha na kujibandika jina la dini, wakajiita: Masufi, na wakaacha kujinasibisha kwa Mtume na Maimamu -alaihimus salaam-, ambao ndio viumbe bora zaidi, hilo likapelekea kwa mashia walio dhaifu kukubali itikadi zao na kufuata na matendo yao waovu, kwa sababu walikuwa wanawalaghai na wanadhihirisha Uchamungu na kupa nyongo duni. Hiyo ni dalili tosha juu ya upotofu wa njia yao hiyo][56].**

Na Shia Imaamiyyah wamepokea hadithi nyingi zinazo tahadharisha mahusiano na kuchanganyika pamoja na Masufi, kwa sababu wao Masufi ndio chanzo cha ushetani na upoteza kwa watu, Masufi wana tabia ya kudhihirisha ufukara na kupanyongo dunia kwa lengo la kuwalaghai wapumbavu na kuwapoteza.

---

55- Abu Ja'far Muhamad bin Sheikh Al-hasan bin Ally Al-hurul 'Aamiliy, mwandishi wa kitabu [Wasaailu Sshia], moja ya vitabu vinane vya kutegemewa vya Shia Ithnaa'sharia.

- Amesema Sheikh Yusuf Al-bahrani kwenye kitabu [Lu'ulatul Bahrain] (Uk. 76). wakati akimuelezea Al-hurrul 'Aamiliy: **"Alikuwa mwanachuoni mtukufu, mtambuzi wa hadithi na Mwana historia".** Tarjamah namba 28.

- Na amesema Al-khonsaniy: **"Sheikh wetu Al-hurrul 'Aamiliy, ni Mwana historia, na ndiye mtunzi wa kitabu: [Wassailus Shia], na ni mmoja kati ya Muhammad watatu katika wanachuoni waliokuja baadae waliokusanya hadithi zote za sheria hii ya Kiislamu".** Tazama kitabu: [Raudhwwt Al-janaat] (Jz. 7, Uk. 96), tarjama namba (605).

56- Kitabu: [Ar risaalatul Ithnaa'sharia fir raddi 'alas Sufiyyah] (Uk. 3).

Mwanachuoni wao mhakiki wa zama hizi Al-mirza Habiibullaah Al-hashimiy Al-khuiy, anaitaja riwaya katika kuwalaani Masufi, na kwamba wao Masufi wamefukuzwa kwenye rehema za Allaah, Anasema: **[Imekubainikia wewe na kukuthibitikia katika ufafanuzi wa hadithi walizo zikitaja kutoka kwa Amiril Mu'miniina (alaihis salaam), kwamba Madhehebu ya Kisufi yote yanakwenda kinyume na madhehebu ya kisheria ya Shia Imaamiyyah, ambayo ndio madhehebu ya haki, -Allaah aimarishe jengo lake, na azitie nguvu nguzo zake na misingi yake.... kama ambavyo pia imekubainikia wewe kwamba zimekuja aya na hadithi nyingi zinazo walaani, kuwakosoa, kuwakosoa, na kuwadharau. Na dalili walizoshikamana nazo kundi hili la bidaa (Masufi), lililofukuzwa na kulaaniwa, ni dalili za uongo...au zenye tafsiri yenye kutatiza, au ni dhaifu.... Ole wao watu waliowafanya watangulizi wao ambao wame-watengenezea wao mwenendo wa bidaa na kuwaghilibu kwa mambo ya upotovu, na wakaridhika na As-shibliy, Al-ghazaliy, Ibnul 'arabiy na Al-juneyd na kuwafanya kuwa ndio Maimamu wao, -Allaah awalaani duniani, na awaongezee wao adhabu huko akhera]**[57].

Na mwanachuoni wao mkubwa wa hadithi na fiqhi Al-hurul 'Aamily ameweka mlango kamili katika kitabu chake: [Ar-risaalat Al-ithnaa'sharia fir raddi 'alas Suufiyyah], na ametaja ndani yake riwaya kadhaa na kauli mbali mbali za kuwakejeli Masufi, na zinazo wajibisha kuwalaani wao na kujitenga nao. Na miongoni mwa hizo ni kauli yake: **[Wamesema baadhi ya masheikh wa shia wenye kuhakiki mambo, katika masheikh wetu wa zama hizi: "Tambua kwamba jina hili la Taswawwuf (Usufi) lilikuwa linatumika na kikundi cha watu waliopotea kuiacha njia ya sawa, kisha likatumiwa baada yao na kikundi wa Wazandiki na watu wapotevu maadui wa Ahlul bayt -alaihimus salaa-, kama vile Al-hassan Al-basriy, Sufyan At-thauriy, n.k.**

57- Kitabu: [Minhaajul baraa'h fiy sharhi Nahjil balaagha] (Jz. 14, Uk. 21).

**kisha wakalitumia waliokuja baada yao na kufuata njia yao, kama vile Al-ghazali, kioongozi wa maadui wa Ahlul bayt, na wala hakuna aliyetumia jina hilo katika Shia Imaamiyyah -alaihimus salaam-, si katika zama za maimamu wala baada yao"]**[58]**.**

## MASUFI MBELE YA SHIA ITH-NAASHARIA NI MAYAHUDI WA UMMA HUU, BALI NI WAPOTOFU ZAIDI KULIKO MAKAFIRI, NA KWAMBA WAO NI WATU WA MOTONI NA AMALI ZAO NI AMALI ZA WATU WAOVU!!

Amenukuu Al-hurul 'Aamiliy katika kitabu chake: "Al-Risaalatul Ith-na asharia fir raddi 'ala Ssuufiyah" (Uk. 16) kutoka kwa Sheikh wake Bahaaud Diyn Muhammad Al-'Aamily katika kitabu chake Al-kashkuul, amesema: Amesema Mtume -Swala na Salamu zimshukie-: **"Hakitasimama kiama mpaka watoke watu katika umma wangu wanaoitwa masufi, sio katika wafuasi wangu, bali hao ni mayahudi wa umma huu, wao ni wapotovu zaidi kuliko makafiri, nao ni watu wa motoni, wanaume wao wananyoa nywele (vipara), na wananyanyua sauti zao kwa kuleta dhikri, wanadhani kwamba wao wapo katika njia ya watu wema, lakini ni watu wa motoni, wanato sauti mfano wa sauti mlio ya punda,…** mpaka akafikia kusema: **na matendo yao ni sawa matendo ya watu waovu"**[59]**.**

Kisha Al-hurul 'Aamily akatoa ufafanuzi juu ya riwaya hii na dalili nyingine alizozitaja katika kuwatia kasoro masufi, akasema: Ninasema: **[Ataye chunguza kauli za wazi zilizotangulia na zinazofuatia, atafahamu kwamba mambo mengi yaliyo muhimu katika dini hayajataja kwa uwazi na kwa msisitizo, hiyo ndio hukumu ya kisheria, kwa sababu ilijulikana kwamba hakuna fitna kubwa kuliko fitna hii, na yenye kuwatatiza watu wengi madhaifu katika Shia Imaamiyyah, kiasi ambacho wale (masufi) waliopita na waliokuja baadae bado wanawadanga watu kwa kudhihirisha kwao ibada na zuhdi (kuipa**

58- Kitabu: [Ar-risaalat Al-ithnaa'sharia fir raddi 'alas Suufiyyah] (Uk. 10).
59- Angalia kitabu: [Al-fusuulul muhimma] (Jz. 2, Uk. 92), na [Wasaailu Sshia] (Jz. 4, Uk. 31).

**nyongo dunia), kisha wakati huo huo wanawapambia wao mambo ya bidaa ambayo yanawatoa wao katika dini ya sawa, na kuwapondoa na njia iliyonyooka, kama vile kuitakidi huluki (Allaah amechanganyika na viumbe wake katika viwiliwili vyao),… mpaka wamewagawa shia Imaamiyyah makundi mawili, kila kundi moja linamtia katika upotevu mwenzie,….Tunajilinda kwa Allaah kutokana na shari ya balaa hili!"**[60].

Na anasisitiza Al-hurrul 'Aamily kwamba zimekuja hadithi nyingi zinazo wakosoa masufi, kuwalaani, na kuwahuku kuwa ni makafiri na wazandiki, kiasi ambacho amekusanya hadithi zaidi ya Elfu Moja ndani ya kitabu chake [Al-ithna asharia fir raddi 'alas Suufiyya] kutoka kwa Mtume -Swala na Salamu zimshukie- na maimamu, **katika kuwakosoa masufi, kuwalaani, kuwakufurisha na kubatilisha kila jambo lao"**[61].

## MSIMAMO WA MAIMAMU WA SHIA ITH-NAASHARIA DHIDI YA MASUFI

### IMAM AS-SWAADIQ ANATOA HUKUMU JUU YA MASUFI, KWAMBA HAO NI MAADUI WA AHLUL BAYT, NA MWENYE KUWAKOSOA NI SAWA NA MTU ALIYEPIGANA JIHAD MBELE YA MTUME -SWALA NA SALAMU ZIMSHUKIE-

Amesema Mwanachuoni wao wa hadithi Abbas Al-Qummi, kwenye kitabu chake [Safiynat Al-bihaar], kutoka kwa Abu Abdillaah As-swaadiq, kwamba mtu mmoja alimuuliza yeye kuhusu watu amabo walidhihiri katika zama hizo, watu hao wanaitwa masufi? Akasema: **[Hao ni maadui zetu, atakaye wafuata hao huyo ni miongoni mwao, na atafufuliwa nao, na watakuja watu watadai kwamba wanatupenda sisi, lakini watawafuata hao, na watajinasibisha nao…. Tambueni kwamba atakaye wafuata hao huyo si katika sisi, nami najitenga nao, na yule mwenye kuwapinga wao na kuwakosoa ni sawa na mwenye kupigana jihadi pamoja na Mtume wa Allaah -Swala na Salamu zimshukie-].**

60- Kitabu: [Ar-risaalat Al-ithnaa'sharia fir raddi 'alas Suufiyyah] (Uk. 16) na (Uk. 34).
61- Kitabu: [Ar-risaalat Al-ithnaa'sharia fir raddi 'alas Suufiyyah] "Muqaddima": (Uk. 3).

## MSIMAMO WA IMAMU AS-SWAADIQ DHIDI YA MASUFI, NA HUKUMU YAKE JUU YAO KWAMBA NI WATU WA ITIKADI POTOFU

Ametaja Al-ardabiily katika kitabu chake **[Hadiyqatu Sshia],** kutoka kwa Imam Abu Muhammad Al-hassan Al-'askariy, kwamba amesema: Aliulizwa Abu Abdillaah As-swaadiq -alaihis salaam- kuhusu hali ya Abu Hisham Al-kufiy? Akasema: **[Alikuwa na Itikadi potofu, na yeye ndiye aliyeanzisha madhehebu potofu ya Tasawwuf, na akaifanya ndio msingi na kituo cha itikadi yake potofu"[62].**

## MSIMAMO WA IMAMU MUSSA BIN JA'AFAR DHIDI YA MASUFI

Amesema Sayyid Hashim Al-bahraaniy katika kitabu chake: [Hilyatul-abraar], kutoka kwa Shaqiq Al-balkhiy amesema: "**Nilihiji nikamuona mtu mmoja mweusi wa rangi amejitenga peke yake hana kitu chochote, akanitazama na akasema: Ewe Shaqiq: (jiepushe na dhana nyingi, hakika baadhi ya dhana ni dhambi), nikajuta na nikasema: Hakika huyu ni mja mwema ameniita kwa jina langu, na akanijulisha yaliyo ndani ya nafsi yangu bila ya mimi kuyasema, nitamuomba radhi pindi nikikutana naye, wakati aliponiona kwa mara ya pili akaniambia,** Ewe Shiqiq: (Hakika mimi ni mwingi wa kusamehe kwa yule aliyeamini na akafanya amali njema na akaongoka Na alipofika Makka nikamuulizia nikaambiwa huyo ni Mussa bin Ja'afar -alaihis salaam-"[63]. Riwaya hii Al-hurru Al-'amily ameifafanua: **[Ninasema: Tazama namna alivyompinga yule aliyemnasibishia yeye Tasawwuf ambayo si ya kisheria, na jinsi alivyomkataza jambo hilo na kumuamrisha ajiepushe nalo, na wala hakuridhika kuitwa jina hili, na alipoitwa jina zuri lenye kuafikiana na sheria alikubali….., ikajulikana kwamba lile jina la mwanzo (Tasawwuf) ni dhambi na upotevu, na ni kitendo kibaya…."[64].**

---

62- Kitabu: [Hadiiqatu Sshia] (Uk. 574).
63- Kitabu: [Hilyatul abraar] cha Al-bahraani (Jz. 2, Uk. 245).
64- Kitabu: [Ar-risaalat Al-ithnaa'sharia fir raddi 'alas Suufiyyah] "Muqaddima": (Uk. 45).

## MSIMAMO WA IMAMU AL-RIDHWA DHIDI YA MASUFI NA HUKUMU YAKE JUU YAO KWAMBA NI WATU WAPOTOFU NA WAJINGA, NA MWENYE KUWAPINGA WAO NI SAWA NA MWENYE KUPIGANA JIHADI DHIDI YA MAKAFIRI AKIWA PAMOJA NA MTUME (SWALA NA SALAMU ZIMSHUKIE)

Ametaja mwachuoni wao Al-ardabiily katika kitabu chake: [Hadiyqat Sshia], kutoka kwa Abu Al-khatab kutoka kwa Imamu Al-ridhwa kwamba amesema: **"Hakuna mtu yeyote mwenye kuamini Tasawwuf isipokuwa kwa ajili ya kufanya hadaa, au upotofu au upumbavu"[65].**

Na katika riwaya nyengine kutoka kwa Abu Al-qasim Ja'afar bin Muhammad Quulawayhi, kutoka kwa Sa'ad bin Abdillaah kutoka kwa Ahmad bin Muhammad bin Issa, kutoka kwa Al-husein bin Said amesema: **"Nilimuuliza Al-ridhwa kuhusu masufi, akasema: Mtu yeyote hawezi kuwa Sufi isipokuwa kwa hadaa au upotofu au upumbavu, na huenda mtu akakusanya yote matatu"[66].**

Na amesema Al-hurrul 'Aamiliy wakati akifafanua hadithi hii na mambo matatu yaliyotajwa (hadaa, upotofi na upumbavu): **"Kama unavyofahamu kwamba Masufi wana mambo ya uzushi, na hii ni kawaida ya watu wote ambao ni maadui wa Maimamu -Alaihis salaam-, kwa hiyo mtu yeyote mwenye kujinasibisha na masufi, ima atakuwa ni katika viongozi, huyo ataingia kwenye kundi la kwanza (hadaa), au ni mtu anayefuata bila elimu, amedanganyika na yale anayoyaona kwao, ataingia kwenye kundi la pili (upotofu), au kwa sababu ya upungufu ufahamu mbaya na kuridhika kwake na dhahiri, huyo ataingia katika kundi la tatu (upumbavu)…"[67].**

Imepokewa kutoka kwa Al-ridhwa kwamba amesema. "Yule ambaye watatajwa mbele yake Masufi kisha hakuwapinga kwa ulimi wake au kwa moyo wake, huyo si katika sisi, **na atakayewapinga ni sawa na aliye**

---

65- Kitabu: [Hadiyqat Sshia: Uk: 15].
66- Kitabu: [Hadiyqat Sshia: Uk: 251].
67- Kitabu: [Ar-risaalat Al-ithnaa'sharia fir raddi 'alas Suufiyyah] "Muqaddima": (Uk. 31).

**pigana jihadi na makafiri akiwa pamoja na Mtume -Swala na Salamu zimshukie-“[(68)].**

Na Al-hurrul ‘Aamiliy ameifafanua riwaya hii kwa kusema: Ninasema: **“Katika riwaya hii kama unavyoona kuna kauli ya wazi juu ya uwajibu wa kuwakemea masufi kwa namna utavyoweza, ukizingatia kwamba kuna dalili za ujumla zenye kuwajibisha kukemea maovu, na ndani yake kuna dalili juu ya ukafiri wao kwa sababu ya kufanana kwao na makafiri, bali inawezekana makusudio yake ya kushabihisha kuwakemea wao ni sawa kupigana jihadi na makafiri…”[(69)].**

************************
*******************

## MSIMAMO WA IMAMU AL-HAADI DHIDI YA MASUFI NA HUKUMU YAKE JUU YAO KWAMBA WAO NI MANASWARA NA MAJUSI WA UMMA HUU

Ametaja Al-ardabiiliy riwaya kutoka kwa Muhammad bin Al-hassan bin Abil-khatwaab amesema: "Nilikuwa na Al-haadi Ally ibn Muhammad -alais salaam- ndani ya msikiti wa Mtume -Swala na Salamu zimshukie-, likamjia yeye kundi katika wafuasi wake akiwemo Abu Hashim Al-ja’afariy na alikuwa ni mtu mwenye ufasaha, na alikuwa na nafasi kubwa mbele yake, kisha wakaingia msikitini kundi la masufi, wakakaa pembeni hali ya kuwa wamezunguka duara, na wakaanza kuleta Tahliil (Laa ilaaha illa Llaahu), akasema -alaihis salaam-: [Msikae pamoja nao hao ni wenye hadaa, hao ni washirika wa shetani wenye kuvunja misingi ya dini, wanafanya zuhudi kwa ajili ya raha tu za miili yao, na wanakesha usiku ili kuziwinda mali za watu, wanashinda na njaa kwa ajili ya kupata rangi nyekundu miili yao, hawaleti adhkaar (Laa ilaaha illaLlaahu) isipokuwa kwa ajili ya kuwahadaa watu, wala hawapunguzi kula isipokuwa kwa ajili ya kuzuia vyungu, na kuzinyakua nyoyo za wanawake wajinga…, nyiradi za oni kuimba, hawawafuati wao isipokuwa watu wajinga, na

68- Kitabu: [Mustadrak al-wasaail] (Jz. 2, Uk. 323).
69- Kitabu: [Ar-risaalat Al-ithnaa’sharia fir raddi ‘alas Suufiyyah] “Muqaddima”: (Uk. 23).

wala hawawaamini wao isipokuwa watu wapumbavu…, **hivi hujui kwamba hilo ndio kundi ovu zaidi la masufi, namasufi wote ni wapinzani wetu, na njia yao ni tafauti nan jia yetu, hawakuwa wao isipokuwa ni manaswara na majusi wa umma huu, wao wanajitahidi kuzima nuru ya Allaah, na Allaah ni mwenye kuitimiza nuru yake ijapo watachukia makafiri"][70].**

Amesema Al-hurrul 'AamilIy wakati akifafanua riwaya hii: "Lau isingekuja kutoka kwao maimamu -Alaihis salaam- isipokuwa hadithi hii tukufu….. yenye kuwatahadharisha masufi na wafuasi wao, na kubainisha wazi upotofu wa kila sufi na ujinga wake, basi ingelitosha katika kubainisha upotevu wao, kwa hakika imebainisha kwa uwazi sana ubaya njia yao…, na kutoa hukumu juu ya ukafiri wao na kutoka kwao katika uislamu. Na jambo hili liko wazi kwa watu wenye akili"[71].

************************************

## MSIMAMO WA IMAMU AL-'ASKARY DHIDI YA MASUFI

Amesema Al-ardabiiliy katika kitabu chake: [Hadiyqat Sshia[72]] na Al-hurrul 'Aamiliy katika kitabu chake [Ar-risalaatul ithnaashiria[73]], kutoka kwa Al-'askary -alaihis salaam- kwamba yeye alizungumza na Abu hashim Al-ja'afary, akasema: "Ewe Abu Hashim, zitakuja zama kwa watu, nyuso zao zitakuwa ni zenye bashasha na nyoyo zao ni zenye kiza na uchafu, sunna kwao ni bidaa, na bidaa kwao ni sunna, muumini kwao hana thamani yoyote, na fasiki kwao ndiye mwenye thamani, viongozi wao ni wajinga madhalimu, na maulama wao ni wenye kwenda kwenye milango ya madhalimu, matajiri wao wanawaibia mafakiri…, **Maulamaa wao ni viumbe wa Allaah wa shari katika mgongo wa ardhi, kwa**

---

70- Kitabu: [Hadiiqatu Sshia] (Uk. 603).
71- Kitabu: [Ar-risaalat Al-ithnaa'sharia fir raddi 'alas Suufiyyah] "Muqaddima": (Uk. 29-23).
72- Kitabu: [Hadiyqat Sshia: Uk. 562].
73- Kitabu: [Ar-risalaatul ithnaashiria: Uk. 33].

**sababu wao wanategemea zaidi Falsafa na Tasawwuf.** Naapa kwa Allaah, hao ni watu waliopinda na Kwenda kombo, wanavuka mipaka katika kuwapenda maadui zetu, na wanawakosoa wafuasi wetu na mawalii wetu"[(74)].

## MAKUBALIANO YA SHIA IMAAMIYYAH JUU YA KUBATILISHA MADHEHEBU YA TASAWWUF NA UKAFIRI WA WAFUASI WAKE

Wameafikiana maulamaa wote wa Shia Imaamiyyah wa zamani na wasasa juu ya kubatilisha madhehebu ya Tasawwuf na kuwasema vibaya wafuasi wake, na kuwaelezea kwa sifa mbaya, na miongoni mwa maulamaa walionukuu makubaliano hayo na kufafanua ni sheikh wao Al-hurrul 'AamilIy katika kitabu chake: [Al-risaalatul Ithnaasharia], baada ya kutaja dalili za kiakili na riwaya kutoka kwa Mtume -Swala na Salamu zimshukie- na maimamu katika kubatilisha Tasawwuf na kuwakashifu wafuasi wake, akataja katika kipengele cha nane ambacho ndani yake alikuwa akielezea Ijmaa (makubaliano ya maulamaa):

Kipengele cha nane: Makubaliano ya Shia Imaamiyyah na mapote yote ya Shia Ithnaasharia, juu ya kubatilisha Tasawwuf na kuwakosoa masufi, tangu wakati wa Mtume -Swala na Salamu zimshukie- na maimamu, mpaka wakati wetu wa sasa… Na wengi katika Ahlus Sunnah Wal-jamaa'h wamewapinga masufi, na mashia wote wamewakataa Masufi, na wamenukuu kutoka kwa maimamu wao hadithi nyingi za kuwasema vibaya masufi…mpaka akasema: **Mashia wote wanaitakidi ukafiri wa masufi, na kuwapinga wao kwa lugha kali…,** na wamepokea kwa maana hii hadithi nyingi kutoka kwa maimamu wao -alaihis salaam-"[(75)].

---

[74]- Kitabu: [Hadiiqatu Sshia] (Uk. 603).
[75]- Kitabu: [Ar-risalaatul ithnaashiria] (Uk. 44-45).

## MSIMAMO WA MAULAMAA WA SHIA IMAAMIYYAH WALIO WAKOSOA MASUFI NA KUWAPA HUKUMU YA UKAFIRI NA UPOTOFU

Miongoni mwa hao:

1. **Sheikh wao Ahmad bin Muhammad Al-adhrabaijany maarufu kwa Al-muqaddas Al-ardabiily** (amefariki mwaka 93h)[76] amewashambulia masufi na kuwaita kwamba ni washirika wa shetani, na wavunjifu wa misingi ya dini, bali ni majusi wa umma huu.

   Amesema Al-ardabiily katika kitabu chake [Hadiyqatu Sshia]: **"Msiwazingatie masufi, kwa sababu wao ni washirika wa shetani na waharibifu wa dini…,** na yeyote atakaye msaidia mmoja wao (masufi) ni kama amemsaidai Yazid, Muawiya, Abaan na Abu Sufiyan"[77].
2. **Sheikh Al-mufid**[78]**,** anasema kuhusu masufi kuwa ni watu wa kuhalalisha kila kitu, bali ni makafiri na wazandiki.

Na miongoni mwa masheikh wakubwa wa Shia Imaamiyah waliotunga vitabu kuwakosoa masufi ni sheikh Al-mufid, anasema Al-hurrul Al-'aamily: "Sheikh Al-mufid Muhammad bin Muhammad bin Nu'uman -Allaah aitakase siri yake-, ametunga kitabu dhidi ya wafuasi wa Al-hallaj, katika kitabu hicho amenukuu wanachuoni wote walio andika katika kuwajibu na kuwakosoa Masufi…, na baadhi ya maulamaa wetu wamenukuu kutoka kwake kwamba amesema: [Tambua kwamba wanachuoni wengi duniani kwa dhahiri ni Shia Imaamiyyah na wanaongea maneno mazuri, lakini wanaficha uovu, wanadhihirisha Imani kwa kutumia taqiyyah na wanaficha ukafiri na uadui, wanakula

---

76- Anaitwa Ahmad Bin Muhammad Aadharbaijaaniy. Amesema Al-hurrul 'Aamiliy kuhusu yeye: "Alikuwa mwanachuoni, mbora, mjuzi wa mambo ya ndani, mtu wa ibada, mwaminifu…". [Amalul Aamal] (Jz. 2, Uk. 23).

77- Kitabu: [Hadiyqat Sshia] (Uk. 564).

78- Anaitwa Abu Abdillaah Muhammad Bin Muhammad Al-'uqbary, amefariki mwaka 1022 milaadiyyah, miongoni mwa maulamaa wakubwa wa Shia Imaamiyyah, amesema mwanafunzi wake Ahmad Bin Ally An-Najaashiy: **"Huyu ni Sheikh wetu na Profesor wetu, fadhila zake zimetangaa katika Fiqh, Hadithi…".** [Mu'jamu rijaali hadiithi] cha An-najashi (Jz. 17, Uk. 202). Na amesema mwanafunzi wake mwingine At-twusi: **"… alikuwa ni mwenye kutangulizwa kielimu na ufundi wa maneno, ni mwanachuoni mkubwa wa fiqh…".**

dunia yao kwa kutumia jina la dini, wanaingiza Shubha kwenye nafsi za waumini dhaifu wa shia, kwa ajili ya kupinga dini ya Allaah na kufanya khiyana kwa jamaa wa Mtume (Ahlul Bayt), kwa hiyo, wakati tulipoona kujipenyeza kwa wafuasi wa Al-hallaaj katika kuwapoteza wafuasi wa kundi lenye kuokoka (Firqatun naajiyah), tukajikita katika kuzuia upotofu wao na kupinga maneno yao, ili wasiweze kuwabadilisha (wafuasi wetu) kwa kuvuka kwao mipaka, na kujitenga na njia ya kuokoka…][79].

Na miongoni mwa maneno aliyosema Al-Mufid kuhusu Masufi: **[Al-hallaajiyyah ni kundi miongoni mwa makundi ya kisufi, nao ni watu wa kuhalalisha (ya haramu), na kuitakidi Huluul[80]…, nao ni Wazandiki na watu wenye kukanusha uwepo wa Allaah…, na wapo mbali na sheria na kuzitekeleza kuliko manaswara na majusi (waabudu moto)][81].**

3. **Na mwanachuoni wao mkubwa Abu Ja'far ibn Baabawaihi (Rais wa maulamaa wa hadithi) amevuka mipaka katika kuwajibu masufi na kuwakosoa.**

Amesema Al-hurrul 'Aamiliy akimuelezea Abu Ja'far na namna alivyotoa juhudi ya kuwakosoa masufi: **"Sheikh mtukufu, Mwenye fadhila nyingi ambazo huweizi kuzidhibiti, kiongozi wa maulamaa wa hadithi, amezaliwa kwa dua ya Swaahib Zzamaan (imamu wa 12 aliyejificha pangoni), amepitiliza katika kuwakosoa wao (masufi), mfano katika kitabu chake: 'Uyuun al-Akhbaar, Ma'ani al-Akhbaar, At-Tawhid, Al-'ilal na vingine, kiasi ambacho amepokea hadithi nyingi za kuwakosoa"**[82].

79- Kitabu: [Ar-risalaatul ithnaashiria] (Uk. 46).
80- Itikadi ya kwamba Allaah amechanganyika kwenye viwiliwili vya viumbe wake.
81- Kitabu: [Tas-hihi I'tiqadaat al-Imaamiyyah] cha Al-Mufid (133).
82- Kitabu: [Ar risaalatul ithnaasharia] (Uk. 48-49).

Na mwanachuoni wao Al-majli[(83)] amekuwa mkali mno katika kuwapinga masufi, na kutahadharisha mafunzo yao. Amesema: […kuna kundi katika watu wa zama zetu wamefanya bidaa kuwa ndio dini, wanamuabudu Allaah kupitia bidaa ya Tasawufi, wakafanya utawa ndio ibada pamoja Mtume -Swala na Salamu zimshukie- amekataza hilo na akawaamrisha watu kuoa.., kisha pamoja na huo utawa wamezua ibada nyingi. Miongoni mwa hizo ni kuleta Adhkaar (dhikri), ambao ni mfumo maalumu kwa mtindo maalumu ambayo hakuna dalili yoyote ya kisheria kutoka katika Qur'an wala hadithi, na mfano wa mambo haya bila shaka ni bidaa tena haramu, na Mtume -Swala na Salamu zimshukie- amesema: "Kila bidaa ni upitevu, na kila upotevu ni njia ya motoni). Na miongoni wa bidaa ni…, kuimba mashairi mfano wa mlio wa punda, kumuabudu Allaah kwa mbinja/miruzi (firimbi) na kupiga makofi, na wanadai hakuna ibada kubwa kuliko mambo haya, na wakaacha ibada zote za sunnah, na wakafupilizika na swala za faradhi kwa kuswali kwa kudonoa kama jogoo (kuswali mbiombio), na lau si kuogopa maulamaa wangeacha kabisa kuswali. Kisha -Allaah awalaani-, hawakutosheka na bidaa hizi tu, bali wamebadilisha mambo ya misingi katika dini, wanaitakidi kwa Allaah ameingia katika viwiliwili vya viumbe wake (wahdatul wujuud), na itikadi nyingine potofu. Tahadahrini enyi ndugu zangu, na ihifadhini dini yenu na imani yenu, na epukeni wasiwasi wa mashetani hawa…, na msihadaike na uwongo wao uliopambwa ambao umewapata watu wajinga…"[(84)].

4. **Ni'imatullaahi Al-jazairiy**[( 85 )] anasema kwamba masufi wamepotea kuiacha njia ya haki.

Anasema kwenye kwenye kitabu chake: "Al-anwaaru Nnu'maaniyyah", chini ya anuani: **(Giza nene katika kubainisha hali za Masufi na**

[83]- Wanamuita Sheikhul Islaam wal-muslimin Muhammad bin Baqir, amefariki 1111h – 1699m.
[84]- Kitabu: [I'tiqadaat Al-majlis] (Uk. 26-29).
[85]- Sayyid Ni'matullaahi Abdullah bin Muhammad Al-jazaairiy, amezaliwa 1050h – 1640m.

**Nawaasib)**[86]:[Tambua kwamba jina hili -la Tasawuf- likitumiwa na wanafalsafa ambao wamepotea kuiacha njia ya haki, kisha baadae likatumiwa na kundi katika Wazandiki][87].

5. **Shihabu-Ddiyn An-Najafiy Al-mar'ashiy**[88], anasema kuhusu Tasawuf na Masufi, ni miongoni mwa misiba mikubwa katika Uislamu.
   Anasema: [Msimamo wangu ni kwamba Tasawuf (Usufi) ndio janga kubwa katika Uislamu, zimetetereka nguzo za Kiislamu na kuingia dosari jengo lake….][89].
6. **Muhammad bin Twahir bin Muhammad bin Hussein Al-shiraziy An-Najafiy Al-qummiy,** amewahukumu Masufi kuwa ni makafiri na wanafiki, amefariki mwaka 1098 h. Bwana huyu huzingatiwa kuwa ni mmoja wa wakosoaji wakubwa wa Tasawuf na wafuasi wake, kama anavyosema mwana Falsafa wa chuo kikuu cha Tehran Doktor Muhsin Jahankiiriy, kwenye kitabu chake: (Muhyid Diyn bin 'Arabiy): [Alikuwa -Muhammad Twahir- ni mtambuzi wa itikadi na kauli za watu wa twariqa, ikiwemo kauli yao ya wahdatul-wujuud (Allaah ameingia katika viwiliwili vya viumbe wake), na akawa mkali katika kulikosoa hilo na kulikataa,… kama alivyokosa mambo mengi katika misingi ya Tasawuf, kama vile itikadi ya wihdatul wujuud na tanzu zake, na akawakufurisha wenye kuitakidi hivyo, bali amesema kuwa ukafiri wao (watu wa twarika) upo wazi zaidi kuliko ukafiri wa Mayahudi na Manaswara][90].
7. **Na As-Shiraazi anaona kwamba ukafiri wa masufi ni mkubwa zaidi kuliko mayahudi na manaswara:** [Haifichiki kwamba watu wa madhehebu haya maovu, ijapo wakijidhihirisha na vazi la uislamu na kuficha unafiki, lakini mbele ya watambuzi kufuru yao ni kubwa kuliko kufuru ya mayahudi na manaswara, kwa sababu wao wanapinga

---

86- Nawaaswib ni maadui wa Ahlul Bayt.
87- Kitabu: [Al-anwaaru Nnu'maaniyyah] (Jz. 2, Uk. 193).
88 - Sayyid Muhammad Hussein Abul Ma'aliy, mmoja kati ya Maulamaa wakubwa wa Shia Imaaamiyyah, amefariki huko Najaf mwaka 1315h.
89- Kitabu: [Ihqaaqu Al-haqqi] (Jz. 1, Uk. 183-185).
90- Kitabu: [Muhyid Diyn bin 'Arabiy] (Uk. 546-547).

Mughayarat (tafauti kati ya kiumbe na muumba), jambo ambalo ni dini zote inalikubali kwa nji ya wajibu...][91].

Na akaendelea As-Shiraziy kutaja kauli za kufuru za Muhyi Ddiyn (Ibn 'Arabi) na kumkosoa mpaka akafikia kusema: [Kuna dalili za wazi juu ya ukafiri wa Ibn 'Arabi kwa kauli zake nyingi za kufuru, na yule ambaye haoni kwamba mwenye kauli hizo ni kafiri na yeye vilevile ni kafiri, … na ametoka kwenye duara la yakini][92].

8. **Na Al-muhaqiq Muhsin Bidarfer ameampa hukumu kila mwenye kujinasibisha na Tasawuf kuwa ni kafiri na ni mzandiki:** [Hakika mtu kujinasibisha na Tasawuf ni sawa na kujinasibisha na ukafiri na uzandiki…][93].
9. **Mwanachuoni wa zama hizi kutoka Lebanon Muhammad Jamil Hamoud Al-'aamiliy,** amebainisha msimamo wa Shia Imaamiyyah dhidi ya masufi, wakati alipoulizwa swali katika chanel yake.

**Akajibu:** [… Tasawuf ni miongoni mwa bidaa za wapinzani (sunni), na maulamaa wetu wamesimama msimamo mkali katika kupinga Tasawuf na Falsafa kwa sababu ya hatari yake…][94].

---

91- Kitabu: [Tuhfatu al Akhbaar] cha As-Shiraziy (Uk. 58).

92- Kitabu: [Tuhfatu al Akhbaar] cha As-Shiraziy (Uk. 165-166).

93- Kitabu: [Haashiyat Kitab ('Ilmu al-Yaqiin fiy Usuuli Ddiyn)] cha Al-faidhul Kaashani. Kwa uhakiki wa Muhsin Bidarfer (Jz. 1, Uk. 37).

94 - Angalia Fat-wa kamili katika: [Markaz al-'atra at-Twaahira] http://www.aletra org/subject.php?id=19

## HAIJUZU KUJIITA SUFI ISIPOKUWA KWA HALI YA KUFANYA TAQIYA[95]

Licha ya ukosowaji wote huo, na kuwakufurisha kwao masufi pamoja na kuwatia katika ufasiki, **lakini wameruhusu mtu kujiita kwa jina lao katika hali ya Taqiya!!**

Imekuja katika kitabu cha (Hadaaiqu Sshia), kutoka kwa Al-ridhwa amesema: [**Hajinasibishi mtu na Tasawuf isipokuwa kwa hadaa, upotofu au ujinga, ama yule atakaejiita kwa jina hilo (sufi) kwa taqiya hana dhambi]**[96]. Na katika riwaya nyengine amezidisha kwa kusema: [Mwenye kujiita **sufi kwa ajili ya taqiyya** hana makosa][97].

Na amefafanua Al-ardabiily kwa kusema: [Alama yake ni kutoshelezeka na kujiita tu, wala asiamini chochote katika itikadi zao za batili][98].

---

95 - Maana ya Taqiya katika lugha ya kiarabu ni: **kuchukua tahadhari**. Ama kwa upande wa Mashia wanakusudia: **Mtu kudhihirisha kinyume na itikadi yako**. Bali ni katika mambo ya msingi katika dini yao.

- Wamenukuu kwamba Ja'far Swadiq amesema**: "Taqiya ndio dini yangu na dini ya wazazi wangu, hana Imani yule asiyekuwa na Taqiya"**. [Usuul al-Kaafi] (Jz. 2, Uk. 217-219).

- Na amesema: **"Lau nilisema: Mwenye kuacha Taqiya ni sawa na mwenye kuacha swala ningelikuwa nimepatia"**. [Man laa yahdhuruhu al-Faqih] (Jz. 2, Uk. 80).

-Amesema Ibn Baabawaihi: **"Taqiya ni wajibu, haifai kuiacha mpaka atoke Qaaim (Mahdi), yeyote atayeacha Taqiya kabla ya kutoka Mahdi, ametoka katika dini ya Allaah na dini ya Imaamiyyah, na amempinga Allaah, Mtume wake na Maimamu wote wa Shia"**. [Al-I'tiqadaat] (Uk. 114-115).

- Bali mwanachuoni wao Al-Hurrul 'Aamiliy katika kitabu chake [Wasaailu Sshia (Jz. 11, Uk. 470)], ameweka mlango maalumu wa Mashia kuishi na Ahlus Sunnah (sunni) kwa Taqiyya, asimdhihirishie itikadi yake ya Ushia, akasema: بَابُ وُجُوبِ عِشْرَةِ العَامَّةِ بِالتَّقِيَّةِ **[Mlango wa uwajibu wa kuishi na sunni kwa Taqiya].**

96- Kitabu: [Hadiyqatu Sshia] (Uk. 251).

97- Kitabu: [Hadiyqatu Sshia] (Uk. 251).

98- Kitabu: [Hadiyqatu Sshia] (Uk. 251).

## HITIMISHO

Imekubainikia ewe ndugu yangu msomaji, uhalisia wa msimamo wa Shia Imamiya dhidi ya masufi, kupitia yale tuliyoonyesha katika maneno ya maimamu wao waliokingwa na Kutenda dhambi (Ma'sumiin), pamoja kutaja kauli za maulamaa wao wenye kutegemewa wa zamani na wa zama hizi.

Kwa mtazamo wa Shia:

- Masufi ni makafiri zaidi ya mayahudi na manaswara.
- Masufi ndio majusi wa umma huu (waabudu moto).
- Masufi ni watu wa motoni.
- Masufi ni watu waliofukuzwa katika rehema za Allaah.
- Jina hilo likitumiwa na watu wapotevu.
- Kisha likatumiwa na wazandiki maadui wa Ahlu bayt.

Hii ndio Tasawuf kwa mtazamo wa Shia na hii ndiyo hukumu yao.

- Je, baada ya kuyajua haya, vipi shia atakudanganya kuhusu umoja?!
- Je, ni kweli mashia hawana uadui na Ahlus Sunnah wote?

Ni matarajio yangu kwamba kila muislamu mwenye akili amefahamu, kwamba mashia wote wa zamani na wasasa msimamo wao ni mmoja dhidi ya masufi, bali dhidi ya Ahlus Sunnah (sunni), na kwamba ukaribu wao kwa Ahlus Sunnah na kutoa misada kwao ni kwa ajili ya Taqiya tu, lakini kwamba wanakubali kuwa wao ni waislamu sahihi.

Swala na Salamu zimshukie Mtume wetu Muhammad, Jamaa zake na Maswahaba wote

## BAADHI YA VITABU VILIVYO ANDIKWA KATIKA KUWAJIBU MASHIA AMBAVYO TUNAWANASIHI WATU KUVISOMA

1. Fatawa za sheikhil Islaam Ibn Taymiyyah.
2. Minhaajus Sunnah (cha Ibn Taymiyyah).
3. Al-milal wan-Nihal (cha Shahrastaniy).
4. Al-farqu bainal firaq (cha Al-baghdadiy).
5. Maqalaat al-Islamiyyiin (cha Al-ash'ariy).

Vitabu vya maulamaa wa zama hizi:

1. Vitabu vyote vya sheikh Ihsaan Dhwahir.
2. Mas'alatu at-Taqrib (cha sheikh D. Nasir Al-qifaariy).
3. Usuul madh-habi Sshia al-ithnaashari'a (cha sheikh Nasir Al-qifariy).
4. Vitabu vyote vya Muhammad Maalullaah.
5. Badhlul majhuud fiy mushaabahati Rrafidhwa lil-yahud (cha Abdullah al-Jamil).
6. Hattaa laa tankhadi' (cha sheikh Abdullaahi Al-mauswiliy).
7. As-shiatul ithnaasharia watakfiiruhum li'umuumil Muslimiin (Abdulaahi As-salafi).
8. Man qatalal Hussein? (cha Abdullahi bin Abdil Aziz).
9. Al-burhaan fiy tabriat Abi Huraira minal buhtaan (cha Abdullaah An-Naasir).
10. Al-intiswaar lil-as'haab wal-Aal (cha d. Ibrahim Ar-Ruheyl).
11. Kashful jaani Muhammad At-tijaniy (cha sheikh Othma Khamis).
12. Bal dhwalalta fiy Rraddi 'alaa abaatwil at-Tijani (cha sheikh Khalid al-'Asqalani).
13. Ma'al ithnaasharia fil usuul wal-furuu' (cha d. Ally As-Salusi).
14. Tabdiidud Dhilaam watanbihun Niyaam… (cha sheikh suleiman Al-Jabhaan).

## MITANDAO MUHIMU YA KUWAJIBU MASHIA AMBAYO TUNASHAURI WATU KUIPITI NA KUISOMA

http//:www.dd-sunnah.net

http//:www.fnoor.com

http//:www.albrhan.com

http//:www.wylsh.com

http//:www.khomainy.com

http//:dhr12.com

http//:www.albainah.net

http//:www.ansar.org

http//:www.almanhaj.com

http//:www.isl.org.uk

http//:www.al-mhdi.com